

25/10/2018

**TAARIFA KUHUSU HALI YA MAFUTA ZANZIBAR**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inapenda kuwajulisha wananchi kwamba Meli Mbili (2) zinazotumika kuleta Mafuta Nchini ,Meli ya United Spirit pamoja na Meli ya Mt Ukombozi zimeharibika na zipo kwenye matengenezo. Meli ya Mt Ukombozi ndio inayotumika kupeleka mafuta katika kisiwa cha Pemba kwa vile ndio inayo weza kufunga nanga na kushusha Mafuta katika Bandari ya Weshu.

Kutokana na kukosekana kwa Meli hiyo, Upelekaji wa Mafuta katika Kisiwa cha Pemba umefanyika kwa kutumia Meli za Mizigo kwa kutumia Magari Maalum kutoka Unguja..

Hali hiyo ilipelekea kasi ya Usambazaji wa mafuta kutoka bohari ya mtoni kwenda kwenye vituo vya mafuta kwa upande wa kisiwa cha Unguja kupungua na kupelekea msongamano wa magari kwenye vituo hivyo.

Hata hivyo Magari yaliyopeleka Mafuta katika kisiwa cha Pemba tayari yamesharudi Siku ya Jumatatu tarehe 22/10/2018 Usiku na yameanza kusambaza mafuta Vituoni kama kawaida, na hali ya upatikanaji mafuta itarejea kama kawaida nchini.

Hali halisi ya uwepo wa mafuta hapa nchini hadi siku ya Alkhamis tarehe 25 Oktoba, 2018 inaonyesha ya kwamba kwa upande wa Kisiwa cha Unguja kuna mafuta ya Petroli lita 403,985 yanayoweza kutumika kwa muda wa siku Tatu (3), mafuta ya Dizeli lita ,813,431 yanayoweza kutumika kwa muda wa siku Tano (5) na Mafuta ya Taa lita 388,444 yanayoweza kutumika kwa muda wa siku Nane (8).

Mbali ya hivyo, Meli ya East Wind imewasili tarehe 24/10/2018 ikiwa na kiasi cha Tani Elfu Moja na Mia Nne (1400 tonnes) za Dizeli sawa na Lita 1,730,000 kutoka bandari ya Mombasa nchini Kenya.

Aidha Meli hiyo baada ya kushusha mafuta inategemewa kurudi tena katika Bandari ya Mombasa na kupakia Mafuta ya Petroli kwa ajili ya matumizi hapa Zanzibar.

ZURA inawaomba radhi wananchi kwa usumbufu uliojitokeza na kuwasisitiza wananchi kuto kusikiliza Taarifa zisizo rasmi ambazo zinazopelekea taharuki.

Matarajio ya ZURA ni kuwa hali ya upatikanaji wa Mafuta Zanzibar itaendelea kuwa nzuri. ZURA pia inawashukuru Wananchi kwa kuwa wastahamilivu na kuwaomba kuendelea kutoa ushirikiano ili kuimarisha huduma za Nishati Nchini.

Naomba kuwasilisha.



.....  
**HAJI KALI HAJI**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**(ZURA)**

